

JARIDA LA

WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANA'A NA MICHEZO



Wizara ya Furaha

TOLEO MAALUM

| 08 Juni, 2021

| www.habari.go.tz

UFUNGUZI WA UMITASHUMTA | UMISSETA 2021



Wizara HabariTZ



Wizara_habaritz




Wizara_HabariTZ



**YALIYOJIRI KATIKA UFUNGUZI
WA MASHINDANO YA MICHEZO
YA UMITASHUMTA NA UMISSETA
MTWARA**

8 Juni, 2021



**TIMU ZA MIKOZA ZIKIINGIA KATIKA UWANJA WA NANGWANDA
SIJAONA KWA AJILI YA UFUNGUZI WA MASHINDANO HAYO
YALIYOFUNGULIWA RASMI NA WAZIRI MKUU WA JAMHURI
YA MUUNGANO WA TANZANIA, MHE. KASSIM MAJALIWA.**





**MGENI RASMI MHE. KASSIM MAJALIWA AKIWASILI
KATIKA UWANJA WA NANGWANDA BAADA YA
KUPOKELEWA NA MKUU WA MKOA MHE. BRIGEDIA
GEN. MARCO GAGUTI.**



**WAZIRI MKUU WA JAMHURI YA MUUNGANO WA
TANZANIA MHE. KASSIM MAJALIWA AKIHUTUBIA
WAKATI WA UZINDUZI WA MASHINDANO HAYO.**



NUKUU ZA WAZIRI MKUU MHE. KASSIM MAJALIWA – Mtwara

“

Napenda pia kuchukua fursa hii kuendelea kuhimiza wito wa Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alioutoa kuwahimiza wananchi kufanya mazoezi ili kuepuka magojnwa yasiyo ya kuambukizwa yanayotokana na mtindo wa maisha tunayoishi. Magojnwa haya yanawagharimu wahusika fedha nyingi katika matibabu na Taifa kwa ujumla katika sekta ya afya. Tuendelee kuunda vikundi vyat mazoezi ya ukakamavu (Jogging na matamasha mbalimbali ya michezo) na kimsingi kujijengea utamaduni wa kufanya mazoezi mara kwa mara kwa afya zenu.

Nisitize tena, Wizara zote husika zikae chini kuangalia Mitaala iliyopo kama inakidhi mahitaji ya sasa na kuchukua hatua stahiki pale ambapo kutaonekana kuna upungufu. Ufundishaji wa somo la Elimu kwa Michezo ufanyike kwa wanafunzi wote na madarasa yote katika Shule za Msingi na kutoa fursa na kuhamasisha wanafunzi wa Shule za Sekondari kusoma somo hilo. Hatua hiyo, siyo tu itatuwekea misingi imara kwa wanamichezo wetu bali itasaidia kupata manufaa mengine kwa watoto wetu kama vile kujenga moyo wa kujiamini, ubunifu, mshikamano na umoja wa kitaifa na kuimarisha afya ya taifa.

MHE. KASSIM MAJALIWA MAJALIWA

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA
NA MICHEZO MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA
AKIMKARIBISHA MHE. WAZIRI MKUU
ILI ATOE HOTUBA YA UFUNGUZI.**



NUKUU ZA WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANA NA MICHEZO MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA – Mtwara

“

Ili kuwa na uendelevu wa vipaji vinavyovumbuliwa katika mashindano haya, Wizara katika kutimiza malengo yake inatarajia kuanzisha kituo maalum cha kuendelezea michezo (Center of Sports Excellency), katika Chuo Cha Maendeleo ya Michezo Malya ili kuendeleza vipaji vinavyopatikana. Kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, tunaendelea kufanya tathimini katika kila mkoa ili kubaini shule zitakazopendekezwa maalum kwa ajili ya kuendeleza vipaji vitakavyotokana na mashindano haya.

Ni matarajio yetu kwa kuisimamia michezo hii vizuri, itakuwa ni chimbuko kubwa la kuvuna vipaji ambavyo vitaendelezwa, ili kupata wachezaji wenyewe weledi, watakaochezea timu zetu za Taifa, lakini pia watakaocheza michezo ya kulipwa, na kujipatia ajira. Ili kufanikisha hilo, tumealika vyama vyote vya Michezo vya Kitaifa, pamoja na vilabu, ili kuja kujionea vipaji katika mashindano haya. Pia tumealika watalaan wa kuvumbua vipaji (scouters), kutoka Taasisi ya Mbwana Samata, pamoja na watalaan kutoka Sweden, ili kuja kuvumbua vipaji.

MHE. INNOCENT LUGHA BASHUNGWA

Waziri wa Habari, Utamaduni, Ssnaa na Michezo.

**MHE. DAVID E. SILINDE NAIBU
WAZIRI OFISI YA RAIS TAMISEMI
AKIMKARIBISHA MHE. BASHUNGWA**



NUKUU ZA NAIBU WAZIRI OFISI YA RAIS TAMISEMI MHE. DAVID E. SILINDE

— Mtwara

“

Lengo kuu la michezo hii ni kutekeleza azma ya Serikali ya kukuza Sekta ya Michezo kwa kuibua, kukuza na kuendeleza vipaji kupitia wanafunzi mashulenii. Michezo ni sehemu ya Taaluma hivyo wanafunzi wanapata fursa ya kushindana, kuibua na kuendeleza vipaji vyao na kujenga Umoja wa Kitaifa, Upendo na Mshikamano.

Katika mashindano ya mwaka huu 2021 jumla ya wanamichezo 3600 kutoka mikoa 26 watashiriki kwenye michezo ya UMITASHUMTA ambapo michezo 10 itashindanishwa. Kwa upande wa jumla ya wanamichezo 3800 kutoka mikoa 28 ya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar watashiriki katika michezo ya UMISSETA.

MHE. DAVID ERNEST SILINDE

Naibu Waziri Ofisi ya Rais – TAMISEMI

**KATIBU MKUU WA WHUSM DKT. HASSAN
ABBASI AKIFUATILIA MPAMBANO WA SOKA
KATI YA MOROGORO NA MBEYA.**



**BAADHI YA WASANII WANAOOTUMBUIZA KATIKA
MASHINDANO YA MICHEZO (UMITASHUMTA
& UMISSETA 2021, MTWARA.**

















UMITASHUMTA | UMISSETA 2021



#MwakaWavipaji

**Limedndaliwa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo
S.L.P 25, 40470 DODOMA, TANZANIA**